BEMBEA YA MAISHA

MASWALI MATARAJIWA KATIKA KCSE

Maswali Matarajiwa Katika Tamthilia ya Bembea ya Maisha katika Mtihani Mkuu wa KCSE

SERIES 2

Ukihitaji Mwongozo Pigia

Bw. Isaboke 0746 222 000 / 0742 999 000

MWALIMU CONSULTANCY

MASWALI

1) ***Teknolojia na maendeleo ni baadhi ya mabadaliko ya lazima katika jamii ya Afrika.*** Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya ***Bembea ya Maisha.***

(alama20)

2) Elimu ni mafundisho muhimu yanayotolewa katika jamii. Jadili kwa kurejelea tamthilia ya ***Bembea ya maisha.***

(alama20)

3) Fafanua mabadiliko yanayojitokeza katika tamthilia ya **Bembea ya maisha**

(alama20)

4) ***La! Kila mbegu ipandwayo haina budi kuzaa na izaapo mazao yake huvunwa. Mtu hutakasa sahani akijua itamfaa tena. Kinacholelewa hakina budi kulea***

a) Eleza mutadha wa dondoo **(alama4)**

b) Chambua mtindo katika dondoo **(alama4)**

c) Kauli iliypigiwa mstari inaonyesha majukumu ya watoto kwa wazazi. Thibitisha kwa kuonyesha wazi alivyowajibika anayerejelewa na msemaji katika mjadala.

(alama4)

d) Tathmini umuhimu wa msemaji katika dondoo hili katika kujenga tamthilia ya **Bembea ya Maisha** **(alama4)**

e) Eleza sifa tano za msemewa katika dondoo hii **(alama4)**

5) Huku ukirejelea tamthilia ya ***Bembea ya Maisha***, eleza tofauti ya hali maendeleo kati ya hospitali za mjini na hospitali za kijijini **(alama20)**

6) Eleza mambo yanayorudisha bara la Afrika nyuma kulingana na tamthilia ya **Bembea ya Maisha** **(alama20)**

7) Eleza namna wahusika mbalimbali wanakabiliana na changamoto zinazowakumba katika tamthilia ya **Bembea ya Maisha** **(alama20)**

8*). 'Nilikupata wapi? Mahututi!'*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

(b) Bainisha mbinu mbili za kimtindo zilizomo kwenye dondoo **(alama2)**

(c) Onyesha toni ya msemaji **(alama2)**

(d) Jadili changamoto alizopitia msemewa wa maneno haya **(alama12)**

9). "***Ninavaa vizuri na kujivisha tabasamu ila ndani viraka na huzuni tele"***

a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

b) Tambua kipengele cha mtindo katika dondo hili **(alama2)**

c) Tambua sifa za msemewa inayojitokeza katika dondoo hili **(alama2)**

d) Eleza mambo yanayomjaza msemaji viraka na huzuni **(alama12)**

10) Eleza nafasi ya mbinu rejeshi katika tamthilia ya **Bembea ya Maisha** kukuza vipengele vifuatavyo:

a) Maudhui **(alama8)**

b) Ploti **(alama8)**

c) Wahusika **(alama4)**

11) ***"Mgaala muuwe na haki umpe"***

a) Eleza muktadha wa dondoo **(alama4)**

b) Tambua kipengele cha kimtindo katika dondoo hili **(alamal)**

c) Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo uliyotaja **(alama2)**

d) Dhibitisha ukweli wa msemaji kwa mujibu wa dondoo hili **(alama3)**

e) Onyesha namna mbinu hiyo ya kimtindo ilivyotumika katika tamthilia ya Bembea ya Maisha **(alama10)**

12) Eleza umuhimu wa wahusika wafuatao katika kujenga tamthia ya **Bembea ya Maisha** **(alama20)**

a) Yona

b) Dina

13) Jadili matumizi ya mbinu zifuatazo katika tamthilia. **(alama20)**

Tashbihi

Istiara

14) Eleza nafasi ya mbinu ya kuchanganya ndimi katika ujenzi wa tamthilia ya **bembea ya maisha** **(alama20)**

15) Kwa kurejelea mifano mbalimbali thibitisha namna ndoa katika tamthilia ya **Bembea ya maisha** zimemulika uhalisia wa jamii za kiafrika. **(alama20)**

16) ***"Lakini nilivyosema, Mungu hamwachi mja wake.."***

a) Eleza mutadha wa dondoo hili **(alama4)**

b) Tambua sifa tatu za msemewa **(alama3)**

c) Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kukuza vipengele vifuatavyo:
Ploti **(alama2)**
Maudhui **(alama4)**

d) Kwa kurejelea tamthilia nzima eleza ukweli wa kauli "Mungu hamwaachi mja wake." **(alama7)**

17) ***Wewe unajua vote valivosemwa. hadharani na faraghani. Si makanisani, si magweni. leo nikiviona vitoto hivi vilivyochekwa na kusimangwa jana, vikijiendeshea mambo yao ninaridhika"***

(a) Bainisha matokeo ya maneno yaliyopigiwa mstari **(alama6)**

(b) Eleza sifa za mwanawe msemewa **(alama4)**

(c) Kwa hoja kumi, jadili namna suala la malezi lilivyoangaziwa katika tamthilia. **(alama10)**

18) ***Naam, bembea! Hata ikiwa ya kamba au chuma hatimaye hulika. Wanasema papo kwa papo kamba hukata jiwe. Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo. Huungwa na mchezo kuanza tena.***

a) Jadili dhana 'bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo. ' Ukirejelea tamthilia **(alama10)**

b) Jadili namna wahusika tofauti wanavyounga bembea **(alama10)**

19) ***"Masombo hufungwa kama walau mtu ametia kitu mdomoni. Pamoja na hali ngumu iliyopo, bado hatujafikia pa kukosa mlo wa kimsingi. Ndiyo hatumudu villiwa vya samli lakini hatuwezi kuishi kana kwamba tunazongwa na nja. Tazama ulivyokonda. Unaelekea kushindana na ng'onda. Hiyo nafasi ya ng'onda unaitaka kwa nini?"***

(alama4)

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili

(b) Onyesha aina moja ya taswira inayojitokeza kwenye dondoo **(alama2)**

(c) Tofauti na taswira, onyesha mbinu mbili za kimtindo zilizomo kwenye dondoo **(alama2)**

(d) Bainisha sifa mbili za msemewa **(alama4)**

(e) Mambo mengi yamebadilika katika jamii. Ukirejelea tamthilia ya Bembea ya maisha onyesha mabadiliko yaliyomo **(alama8)**

20) ***"Unayafanya makubwa bure mwenzangu. Unafahamu vizuri kuwa hiyo si hulka yangu. Sasa mimi nina haja gani kuuvunja mji?"***

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

(b) Bainisha toni ya msemaji **(alama2)**

(c) Msemaji amepitia dhiki mbalimbali katika jamii yake, Tambua dhiki alizopitia **(alama4)**

(d) Onyesha namna maudhui ya mgogoro yanavyojitokeza katika tamthilia nzima **(alama10)**

21) ***Yule tangu akiwa kiduchu amekuwa na kimo cha sindano ya nguo lakini vilevile mwenye akili ncha ya sindano. Nilipomwona mwisho alikuwa bado vilevile lakini bado vilevile lakini akikutazama unahisi anzisoma fikra zako.***

a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

b) Kwa kutoa mifano taja mtindo unazojitokeza katika dondoo hili **(alama12)**

c) Taja sifa nne ya msemaji inayojitokeza katika dondoo hili **(alama4)**

22) ***Ndoa ni bembea. Kuna wakati itakuwajuu na wakati itakuwa chini. Hizo juu — chini chini — juu ndizo utamu wake. Ni kama maisha kwa jumla. Yanapandashuka ndiyo lakini pandashuka hizo ndizo hutupa kuridhika hatimaye tunapozishinda.***

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama4)**

(b) Eleza sifa nne za msemewa **(alama4)**

(c) Jadili namna wahusika tofauti wanavyocheza bembea kwa zamu. **(alama12)**

For Marking Schemes/Answers

Contact Mr Isaboke

THE END

SET BOOKS AVAILABLE WITH US

- ✓ ***Artist Of The Floating World***
- ✓ ***Bembea Ya Maisha***
- ✓ ***Mapambazuko Ya Machweo***
- ✓ ***Nguu Za Jadi***
- ✓ ***Fathers Of Nations***
- ✓ ***Silent Songs And Other Stories***
- ✓ ***A Parliament Of Owls***
- ✓ ***The Samaritan***
- ✓ ***Cheche za Moto***

OTHER SETBOOKS GUIDES AVAILABLE				
SETBOOK	**GUIDE**	**QUESTIONS & ANSWERS**	**VIDEOS**	**CONTACT**
Bembea Ya Maisha	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Mapambazuko Ya Machweo	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Nguu Za Jadi	✓	✓	✓	*0746-222-000*
	ENGLISH SETBOOKS			
Fathers Of Nations	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Silent Songs And Other Stories	✓	✓	✓	*0746-222-000*
A Parliament Of Owls	✓	✓	✓	*0746-222-000*
The Samaritan	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Artist Of The Floating World	✓	✓	✓	*0746-222-000*

FOR THE FOLLOWING;

- ✓ ONLINE TUITION
- ✓ REVISION NOTES
- ✓ SCHEMES OF WORK
- ✓ SETBOOKS VIDEOS
- ✓ TERMLY EXAMS
- ✓ QUICK REVISION KITS
- ✓ KCSE TOPICALS
- ✓ KCSE PREMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREMOCKS
- ✓ JOINT PREMOCKS
- ✓ KCSE MOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS MOCKS
- ✓ JOINT MOCKS
- ✓ KCSE POSTMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREDICTIONS
- ✓ KCSE PREDICTIONS
- ✓ KCSE REVEALED SETS

CALL/TEXT/WHATSAPP

0746 222 000

mwalimuconsultancy@gmail.com

This is a Copyright Property of Mwalimu Consultancy Ltd.

POWERED BY MR ISABOKE

SUCCESS

REGARDS